# SIGNS AND TOKENS

## ISHARA NA VITENDO VYA IMANI VYENYE KUZALISHA MATOKEO

**Pastor Tony Osborn**



**© May 2024 Pastor Tony Osborn**

Kitabu hiki kimeandikwa na **PASTOR TONY OSBORN**. Haki zote zimehifadhiwa, huruhusiwi kunakili, kurudufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

Kufanya hivyo itakuwa ni Ukiukwaji wa taratibu na hii inaweza kukupelekea kushtakiwa kutoka kwa waandaaji wa kazi hii.

**Pastor, Tony Osborn**

**Dar es salaam, TANZANIA (Afrika Mashariki)**

**Simu: 0762153539/0659085731**

**Instagram / Tiktok: Pastor Tony Osborn**

**ISBN: 978-99112-9811-5-**7

Kwa Ajili Yako.
**(Present to you)**

Kutoka Kwa.
**(From)**

**YALIYOMO: SHUKRANI ...** Error! Bookmark not defined.

**UTANGULIZI ............................................................... x**

KUSUDI LA KUANDIKA KITABU HIKI**........................xi**

***Sura ya Kwanza. .......................................... 1***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MCHANGA/ UDONGO .......................................... 1

MAOMBI YA KUFUFUKUA CHOCHOTE CHA KWETU KILICHOMEZWA NA KUZIKWA NA ARDHI. ........................................................... 9

MAOMBI YA KUPANDA MBEGU NJEMA JUU YA ARDHI NA KUIAMURU KUTII YALE YOTE UTAKAYOYATUMA. .................................. 12

MAOMBI YA UKIRI JUU YA ARDHI. ....................... 14

***Sura ya Pili. .................................................. 16***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MAJI. ........... 16

MAOMBI YA KUYAOMBEA MAJI KUWA DAMU YA YESU INENAYO MEMA. ................... 24

MAOMBI YA KUTENGA VITU VYAKO KWA KUTUMIA DAMU YA YESU ................................. 25

MAOMBI YA UKIRI JUU YA MAOMBI ULIYOFANYA KWA KUTUMIA DAMU

YA YESU ........................................................................ 28

***Sura ya Tatu. .................................................. 29***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA KARATASI............................................................. 29

MAOMBI YA KUFUTA NA KUAHIRISHA TAARIFA NA HABARI ZOTE MBAYA. ............... 40

MAOMBI YA KULETA HABARI NA TAARIFA NZURI KATIKA MAISHA YETU ....................... 43

MAOMBI YA KUWATANGAZIA WATU WOTE WALIOPANGA KUTUANDIKIA BARUA ZENYE HABARI MBAYA. ..................................... 45

MAOMBI YA UKIRI KWA TENDO LA IMANI TULILOFANYA KWA KUTUMIA KARATASI. ........................................................ 54

***Sura ya Nne. .................................................. 55***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MAKUFULI. ........................................................... 55

MAOMBI YA KUFUNGUA KILA KIFUNGO KILICHOKUSHIKILIA........................................ 59

MAOMBI YA KUFUNGA KILA HALI MBAYA NA MAMBO MABAYA MAISHANI MWETU ...... 63

MAOMBI YA UKIRI KWA TENDO LA IMANI TULILOFANYA KWA KUTUMIA MAKUFULI 66

***Sura ya Tano. ................................................ 67*** TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA CHUMVI NA MAFUTA. ........................................................ 67

Namna ambavyo Chumvi hutumika ulimwengu wa Roho ............................................................ 67
Namna ambavyo mafuta hutumika ulimwengu wa Roho ............................................................ 69

MAOMBI KWA KUTUMIA CHUMVI. .................. 73

MAOMBI KWA KUTUMIA MAFUTA. ................. 75

MAOMBI YA UKIRI KWA TENDO LA IMANI TULILOFANYA KWA KUTUMIA CHUMVI NA MAFUTA. ........................................ 77

***Sura ya Sita. ...................................................... 78***
TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA JIWE. ......... 78

***Sura ya Saba. .................................................... 83***
TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MSHUMAA. ............................................................ 83

MAOMBI YA KUWASHA TAA ZETU ILI ZIANGAZE. .......................................................... 88

MAOMBI YA UKIRI KWA TENDO LA IMANI TULILOFANYA KWA KUTUMIA MSHUMAA. ....................................................... 90

***Sura ya Nane. ............................................... 91***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA UPEPO ...... 91 ***Sura ya Tisa. ................................................. 94***
TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA KIATU....... 94

MAOMBI YA IMANI KWA KUTUMIA VIATU NA MIGUU YETU ................................... 98

MAOMBI YA UKIRI KUPITIA TENDO LA IMANI LA KIATU TULILOFANYA;. ................ 100

**HITIMISHO: ........................................................ 101**

# SHUKRANI:

Ninamshukuru Mungu sana kwa uaminifu wake na kwa kunijalia ROHO MTAKATIFU ambaye kwa mafunuo yasiyo ya kawaida amenipa NEEMA ya kuandika kitabu hiki kilichobeba mafunuo na siri nyingi sana juu ya somo zima la ishara na vitendo vya kiimani ambavyo vinaweza kubadilisha maisha ya mtu.

Siri zilizoandikwa humu kwa uwezo wa Roho wa Mungu zitakusaidia na kukuongoza hatua kwa hatua namna ya kutumia ishara na matendo ya kiimani yaliyomo humu ili kupata ukombozi katika kila eneo la maisha yako na kuweza kukuinua katika ukuu ambao Mungu alikuita.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

**Marko 16:17-18**

**"Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya."**

Kwahiyo ishara na matendo ya kiimani sio jambo jipya bali ni jambo ambalo Yesu mwenyewe aliliruhusu kwetu ili kuweza kuona na kupata matokeo tunayoyatamani maishani mwetu.

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa mafunuo wa mafundisho ya Kiimani ambayo yatatuhusisha sisi kufanya vitendo vya kiimani kwa kutumia vitu ambavyo Mungu mwenyewe aliviumba ili kuleta matokeo katika maisha yetu.

Kama vile Neno la Mungu linavyosema katika kitabu cha;

**Yakobo 2:7**

**“Vivyo hivyo, imani peke yake bila matendo imekufa.”**

Kwahiyo ili imani zetu ziwe na matokeo lazima ziambatane na matendo. ***Matendo gani?*** Utajifunza zaidi katika kitabu hiki.

Shukrani zangu za pekee ziwafikie watoto wangu wa kiroho wote, ndani na nje ya nchi ya Tanzania, kwa kunipenda, kuniombea na zaidi ya yote kunipokea na kuniamini na kwa Kumuamini Mungu aliyeniita na huduma iliyopo ndani yangu.

Ninawashukuru sana kwa kuwa nyie mmenipa nafasi katika mioyo yenu na kuamini kile kitu na huduma Mungu ameweka ndani yangu.

Ninawapenda, ninawaombea na Mungu wa mbinguni awabariki sana.

Kiupekee kabisa ninamshukuru mke wangu mpenzi Mrs Neema Tony Kapola ambaye amekuwa akikesha pamoja nami, akisukuma na kusimamia kwa ufasaha ukamilifu wa kitabu hiki. Ninakupenda na Asante kwa kusimama na mimi katika wito na kazi hii ambayo Mungu amenipa.

Mungu aendelee kukuonekania wewe na familia yako ndani ya mwaka huu.

Amen……………………

**-Pastor Tony Osborn**

# UTANGULIZI:

Katika Biblia tunaziona na kuzisoma habari za manabii, mitume na watumishi mbalimbali wa Mungu na moja ya kitu kikubwa kilichotawala katika kipindi hiko ni ishara na vitendo vya Kiimani ambavyo katika hivyo jina la Mungu lilitukuzwa sana.

Ishara na vitendo vya imani vilivyofanyika ilikuwa ni njia mojawapo ya kumtambulisha Mungu ndani ya maisha ya mtu.

Namaanisha, kutokana na zile ishara na matendo ya imani yaliyofanyika watu waliweza kumjua Mungu na kuamini uwepo wake.

Kila kitendo cha imani kilichofanyika kilipelekea Mungu kusifiwa na kujulikana na wale wasiokuwa wamemjua au kumuamini.

Kabla sijaelezea kiundani sababu au kusudi la kuandika kitabu hiki, tuangalie mifano michache ya watu wa Mungu katika Biblia ambao walifanya vitendo vya kiimani na ishara ambazo zilifanya Mungu atukuzwe na kuogopwa na wao kufanikiwa.

i. **Eliya (Aliizuia Mvua kunyesha na Manabii wa Baali)**
**1 Wafalme 17:1-2**
ii. **Joshua (Alisimamisha Jua)**

**Joshua 10:12-15**

iii. **Musa (Alitumia fimbo kufanya ishara na maajabu)**

iv. **Elisha (Alitumia chumvi kuiponya nchi) 2 Wafalme 2:19-22**

v. **Yesu (Alitumia mate na matope kumponya mgonjwa wa upofu)**

## KUSUDI LA KUANDIKA KITABU HIKI:

Kitabu hiki nimekiandika nikiwa na kusudi la kuwasaidia watoto wa Mungu kuziambatanisha imani zao na vitendo ili ziwaletee matokeo halisi.

Nimegundua kuwa watu wengi hasa waliookoka wana Imani kubwa sana lakini kwa sababu ya kushindwa kuambatanisha imani zao na matendo basi wanabakia kuamini pasipo kuona matokeo ya imani zao.

Mfano; Kama unaamini utapata kazi katika kampuni fulani ni matendo gani uyafanye ili kuonyesha kweli wewe umeamini?

Kama unaamini utaolewa, nini ufanye kitakachoonyesha ulimwengu wa roho kuwa kweli wewe umeamini?

Malaika hawatendei kazi maneno yako ya imani au machozi yako unayolia yanayoonyesha kuwa umeamini. Bali hufanyia kazi vitendo vinavyoambatana na imani yako.

Yaani, kusema una imani au kuamini peke yake haitoshi bali inakuhitaji wewe uambatanishe imani yako na matendo ili kuona matokeo.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha:

**Yakobo 2: 14-23**

**“Ndugu zangu, kuna faida gani mtu kusema ana imani, lakini haonyeshi kwa vitendo? Je, hiyo imani yawezaje kumwokoa?**

**Tuseme kaka au dada hana nguo au chakula.**